JAMHURI YA MUUNGANO WATANZANIA

**OFISI YA RAIS -TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

**HALMASHAURI YA WILAYA YA CHATO**

**MKUU WA SHULE 0755375359/0738077311,**
**MAKAMU MKUU WA SHULE: 0745060121,**
**PATRON: 0629721814,**
**SHULE YA SEKONDARI MUUNGANO BOYS,**
**S. L .P 116, CHATO,**
**Tarehe 1/5/2024.**

EMAIL: muunganoboyssec@gmail.com

**Kumb.Na.CSS/ADM/F.V/2024/2025**
**MZAZI/MLEZI WA**

**…………………………………………………………………….**

**YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI MUUNGANO BOYS HALMASHAURI YA CHATO MKOA WA GEITA MWAKAWA MASOMO 2024/2025**

Ninayo furaha kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na kidato cha tano katika shule hii

**MCHEPUO WA: HGL……..HGK……..HKL………..PCB …….. HONGERA NA KARIBU SANA.**

1. **MAHALI SHULE ILIPO**

Shule ya sekondari Muungano Boys ipo mkoani Geita wilaya ya Chato umbali wa kilometa takribani 10 kutoka stendi kuu ya mabasi **Kahumo**. Shule ipo jirani na Shule ya Msingi Rubambangwe. **Utaona kibao cha shule barabarani mara tu utakapofika shule ya msingi RUBAMBANGWE.**

**NAMNA YA KUSAFIRI KUFIKA SHULENI**

- Kwa wanaotoka mkoa wa Kigoma au wilaya ya Ngara,wapande magari ya kwenda Mwanza ,wateremkie Bwanga na hapo wapande magari ya kuja Chato wateremkie stendi kuu ya mabasi Kahumo na kuchukua bajaji au bodaboda kuja shuleni.
- Wanaotoka mkoa wa Kagera wilaya za; Bukoba,Karagwe,Muleba wapande magari ya kwenda Mwanza wateremkie **kwa MAGUFULI** kisha wapande bajaji au pikipiki iwalete shuleni.
- Biharamulo wapande magari ya Chato, wateremkie **kwa MAGUFULI** kisha wapande bajaji au pikipiki iwalete shuleni.
- Kwa wanaotoka mikoa ya Mara, Arusha, Simiyu, Dodoma, Singida, Manyara, Kilimanjaro, Dar es salaam, Mbeya, Tanga, n.k wapande magari yanayokwenda Mwanza, wakifika Mwanza wapande magari yaendayo Bukoba wateremkie **kwa MAGUFULI** kisha wapande bajaji au pikipiki iwalete shuleni.

**Nb:Ikiwa Utashushiwa Stendi Kuu (Kahumo) Panda Bajaji Au Pikipiki Ikulete Shuleni. Kwa maelekezo zaidi piga simu zetu.**

**2. UENDESHAJI WA SHULE**
Shule hii inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya Elimu Na.25 ya mwaka 1978, pia inazingatia miongozo yote inayotolewa na wizara yenye dhamana ya elimu nchini

Hivyo kwa kipindi chote mwanao atakapokuwa mwanafunzi wa shule hii, atatakiwa kufuata na kuheshimu sheria,kanuni na taratibu zote za shule akiwa ndani na nje ya shule **kwani atakuwa akiiwakilisha shule popote atakapokuwa.**

**NB: Kutokujua sheria hakutakuwa kinga ya kutokuchukuliwa hatua stahiki**.

**3. MAVAZI UTAKAPOKUWA SHULENI**

**A.** Wakati wote wa muda wa masomo mwanafunzi anatakiwa kuvaa sare ya shule ambayo ni **SURUALI DARK GREEN(KIJANI JESHI), SHATI NYEUPE** (**mikono mirefu**) **TAI ya shule na SWETA.**

B. Wakati wote nje ya muda wa masomo mwanafunzi anatakiwa kuvaa **SURUALI DARK BLUE** na **T-SHIRT** ya shule.

C. Siku za sikukuu, Jumamosi na Jumapili, mwanafunzi anatakiwa kuvaa **SURUALI DARK BLUE** na **T-SHIRT** ya shule.

**D. TRACKSUIT (DARK GREEN) itavaliwa wakati wa masomo ya usiku (prep) au kwenye ziara za kimichezo.**

**E.** Wakati wa michezo na wakati wa usafi wa mazingira **mwanafunzi atavaa BUKTA na T-SHIRT YAKE (RANGI NYEUSI)**

**NB: Kwa sababu yoyote ile mwanafunzi haruhusiwi kumiliki au kuvaa nguo za kiraia (ASIJE NAZO KABISA).**

Pamoja na barua hii naambatisha viambatisho vifuatavyo. (a) Orodha ya mahitaji,(b) Mchanganuo wa malipo.(c)sheria za shule,(d) Fomu ya kiapo,(e)Fomu ya taarifa binafsi ya mwanafunzi,(f) Fomu ya hospitali. g)kiambatisho cha ziada

**4. KURIPOTI SHULENI**
Mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni kuanzia tarehe **1/7/2024** na mwisho wa kuripoti ni tarehe **14/7/2024**

**ANGALIZO;**
**Malipo yote yafanyike tawi lolote la benki ya NMB AU MAWAKALA kupitia akaunti za shule zilizotolewa katika kiambatisho (b). Tafadhali ANDIKA JINA LA MWANAO KWENYE RISITI YA BENKI WAKATI WA WALIPO ILI LISOMEKE KWENYE BANK STATEMENT KURAHISISHA UFUATILIAJI WA MICHANGO.**

**ASANTE**

………………………………
**MKUU WA SHULE**

MKUU WA SHULE
MUUNGANO BOYS SEC. SCHOOL
S.L.P 6 CHATO

*Kiambatisho (a)*

**HALMASHAURI YA WILAYA YA CHATO SHULE YA SEKONDARI MUUNGANO BOYS**

## MAHITAJI

### A. MAVAZI

| SN | VAZI | RANGI | IDADI |
|---|---|---|---|
| 1 | SURUARI | DARK GREEN-KITAMBAA KRIETA No 1(inapatikana shuleni) | 2 |
| 2 | SURUALI | DARK BLUE-KITAMBAA KRIETA No 1(inapatikana shuleni) | 2 |
| 3 | SHATI | NYEUPE AINA YA TOMATO (MIKONO MIREFU) | 2 |
| 4 | T-SHIRT YENYE NEMBO YA SHULE | RANGI YA GOLD(inapatikana shuleni) | 1 |
| 5 | VIATU | VYEUSI (VYA KAMBA, VISIGINO VIFUPI) | JOZI 2 |
| 6 | MKANDA | MWEUSI WA NGOZI (USIWE NA UREMBO) | 1 |
| 7 | SOKSI | NYEUSI | JOZI 2 |
| 8. | SWETA YENYE NEMBO YA SHULE | BLUE – (inapatikana shuleni) | 1 |
| 9 | RABA | NYEUPE KABISA | JOZI 1 |
| 10 | TRACKSUIT | DARK GREEN (inapatikana shuleni) | JOZI 1 |
| 11. | T-SHIRT NA BUKTA YAKE | DARK GREEN(inapatikana shuleni) | JOZI 1 |
| 12 | TAI | DARK GREEN MICHIRIZI MYEUPE(inapatikana shuleni) | 1 |
| 13 | VIATU VYA MICHEZO(Njumu) | Rangi yoyote (Kwa wachezaji wa mpira wa miguu tu) | |
| | | | |

### B. MALAZI

a) Godoro imara futi 2½ kwa futi 6.
b) Shuka 'pair' 2 rangi ya **BLUU BAHARI** kwa ajili ya kutandika na kujifunika.
c) Chandarua ya duara au pembe nne 4/6'' rangi ya bluu
d) Foronya/mto rangi ya bluu pamoja na blanketi kwa wenye uhitaji huo.

### C. MAHITAJI MENGINE

| SN | HITAJI | MCHEPUO | IDADI |
|---|---|---|---|
| 1 | NDOO NDOGO Lt.10 | PCB, HKL, HGL,HGK, HGFa, HGLi | 1 |
| 2 | BRUSH KUBWA(HARD BROOM) UKIPATA ZA TANZANIA NI IMARA ZAIDI | HKL | 1 |
| 3 | BRUSH NDOGO YA KUSUGULIA SINK LA CHOONI | HGK | 1 |
| 5 | MOPA (MOPPER) (HGL | HGL | 1 |
| 6 | JEMBE LENYE MPINI WAKE | PCB | 1 |
| 7 | KWANJA | HGLi, HGFa | 1 |
| 8. | RIMU YA KARATASI NYEUPE A4 1 KWA MWAKA(inapatikana shuleni) | PCB, HKL, HGL,HGK, HGFa, HGLi | 1 |
| 9 | RULED PAPER, 1 KWA MWAKA (inapatikana shuleni) | PCB, HKL, HGL,HGK, HGFa, HGLi | 1 |
| 10 | SPRING FILE/PLASTIC FILE | PCB, HKL, HGL,HGK, HGFa, HGLi | 1 |
| 11 | KIKOKOTOZI (SCIENTIFIC CALCULATOR) | PCB | 1 |
| 12 | DISSECTING KIT | PCB | 1 |
| 13 | COUNTER BOOKS Q4 au Q3 | PCB, HKL, HGL,HGK, HGFa, HGLi | 7 |
| 14 | SABUNI YA MAJI KWA AJILI YA USAFI CHOONI Lt 1.5 | PCB, HKL, HGL,HGK, HGFa, HGLi | 1 |

**NB: KILA MWANAFUNZI AFIKE NA NAKALA ZIFUATAZO:**

- **Nakala ya cheti cha kuzaliwa (LAZIMA ALETE) (siyo kadi ya kliniki).**
- **Nakala ya taarifa ya matokeo  kidato IV (result slip)**
- **Passport size 4 (mbili zakwake na mbili za mzazi au mlezi)**

*Kiambatisho (b)*

**HALMASHAURI YA WILAYA YA CHATO SHULE YA SEKONDARI MUUNGANO BOYS**

# MICHANGO YA SHULE

Michango ifuatayo iwekwe katika akaunti ya shule inayoitwa **"MUUNGANO BOYS SECONDARYSCHOOL RECCURENT ACCOUNT"** Na. **32710025254 NMB** :

| **Na** | **AINA YA MCHANGO** | **KIASI** |
|---|---|---|
| **1** | MCHANGO WA UENDESHAJI WA SHULE | 65,000 |
| **2.** | NEMBO | 5,000 |
| **3.** | TAHADHARI | 5,000 |
| **4.** | KITAMBULISHO CHA SHULE | 5,000 |
| | **JUMLA KUU** | **80,000** |

**Angalizo: Fedha zote zilizoainishwa katika jedwali hapo juu hazitapokelewa TASLIMU. Wasilisha slip ya bank na hakikisha unapewa risiti yako kutoka ofisi ya uhasibu.** ***Kwa ufafanuzi endapo utapata utata piga NAMBA ZA SIMU zilizotolewa katika anwani hapo juu.***

## MATIBABU.

**Mzazi/mlezi ni vema ukatambua kuwa swala la matibabu kwa mwanao ni jukumu lako, hivyo tunapendekeza mambo yafuatayo:**

I. **Tafadhali mkatie bima ya afya (NHIF) mwanao, NA UMPATIE AJE NAYO WAKATI WA KURIPOTI.**

II. **Serikali imeweka utaratibu wa bima ya afya iitwayo "CHF iliyoboreshwa", ambapo watoto sita wataunda familia moja na kulipia 5,000 kila mmoja KWA MWAKA kwa ajili ya kupata huduma za hospitali kupitia bima hii. Waweza kuchangia hii kama hutaweza kupataNHIF. Fedha hiyo aje nayo mkononi wakati wa kuripoti.**

III. **Ikiwa utaratibu wa hapo juu utashindikana na huduma ya kwanza itakayotolewa kwa mtoto haitakuwa msaada, basi utalazimika kulipia gharama za matibabu zitakazojitokeza.**

**NB: Kwa mzazi ambaye anafahamu afya ya mtoto wake inahitaji uangalizi wa karibu sana, tunashauri afanye utaratibu wa kuomba kubadilisha kituo mapema kabla utaratibu wa kuanza kuripoti haujaanza.**

*Kiambatisho (c )*

**HALMASHAURI YA WILAYA YA CHATO**
**SHULE YA SEKONDARI MUUNGANO BOYS**

# SHERIA ZA SHULE

**(a) TARATIBU NA KANUNI ZA SHULE**

1. **HESHIMA**: Kila mwanafunzi anatakiwa kwanza kujiheshimu mwenyewe, kuwaheshimu walimu,wazazi/walezi,wageni na viongozi kwa ujumla.
2. **MAWASILIANO**: Kingereza ndiyo lugha pekee ya mawasiliano hapa shuleni,hivyo mwanafunzi haruhusuwi kuasilina kwa lugha nyingine yoyote isipokuwa tu wakati wa midaharo ya Kiswahili.
3. **USAFI**:Kila mwanafunzi anatakiwa kutunza usafi wa mwili na mazingira ya shule kwa ujumla.

4. **RATIBA YA SHULE**: Kila mwanafunzi anapaswa kuheshimu ratiba ya shule.Mwanafunzi haruhusiwi kuwa nje ya mazingira ya shule bila ruhusa maalum kutoka kwa uongozi wa shule. Aidha mwanafunzi anatakiwa kuwahi darasani na katika shughuli mbalimbali za shule ikiwa nipamoja na kutii wito (**kengere.)**

**(b) MAKOSA YA KUMFUKUZISHA MWANAFUNZI.**

1. Wizi wa aina yoyote. 2.Uasherati, ushoga na ubakaji
3. Ulevi wa pombe/madawa ya kulevya kama vile mirungi,kuber,bangi n.k
4. Kupiga/kupigana/kutoa lugha chafu kwa wanafunzi/walimu/jamii5.Kuharibu kwa makusudi mali ya umma
6. Kudharau bendera ya Taifa
7. Kuoa/kumpa mimba msichana
8. Kugoma,kuchochea/kuongoza mgomo na kuvuruga amani na usalama shuleni /jamii
9. **Mwanafunzi kumiliki line/simu ya mkononi**
10. Udanganyifu wa aina yoyote katika mitihani11.Kugomea adhabu yoyote halali
12. Kutotii serikali iliyopo madarakani na chama tawala
13. Kuwa nje ya shule bila sare ya shule na bila ruhusa/kibali maalum kutoka kwa uongozi wa shule
14. Kuonekana kwenye nyumba za wageni na kumbi za starehe
15. Utoro/kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku tisini bila taarifa

***Angalizo:Mwanafunzi HARUHUSIWA KUMILIKI SIMU SHULENI atakayebainika/kukamatwa na simu atatozwa faini ya shilingi lakimbili tu (Tsh.200,000/=) Hivyo mzazi mwonye mwanao maana itasaidiakuepuka kuisababishia familia hasara isiyo ya lazima.***

**Kwa kuwa mwanafunzi harusiwi kumiliki line/simu, shule imeweka utaratibu kwa wazazi/walezi kuwasiliana au kuwatumia watoto wao fedha ya matumizi kupitia simu maalumu ya shule**

**PIA**: Mwanafunzi harusiwi kumiliki vifaa vya umeme kama vile pasi,heater,n.k. Aidha mwanafunzi harusiwi kumiliki redio yenye kubeba memory card/frash**. Atakayebainika kumiliki vifaa hivi atatozwa faini ya kununua vifaa vya umeme vitakavyopendekezwa na kamati ya nidhamu/bodi ya shule.**

*Kiambatisho(d)*

# HALMASHAURI YA WILAYA YA CHATO

**SHULE YA SEKONDARI MUUNGANO BOYS,**
**S.L.P 116,**
**CHATO.**

**TAREHE............................**

**KUMB.NA.CSS/ADM/FV/2024/2025**

## FOMU YA KIAPO

Mzazi/Mlezi wa (Jina la mwanafunzi)

______________________________

Mimi..........................................(mwanafunzi) bila shuruti nakubali kutumia nafasi niliyopewa ya kidato cha ...............katika shule ya sekondari Muungano Boys. Pia nimesoma na kuelewa maelekezo yote yaliyomo katika fomu hii,naahidi kuyazingatia **yote** ikiwa ni pamoja na kufikisha **wastani wa shule wa 60%** katika mitihani ya ndani na nje kwa mafanikio yangu kitaaluma na kutokushiriki kwa namna yoyote ile katika migomo na maanadamano yasiyoruhusiwa.

........................... ...................

Saini ya mwanafunzi Tarehe

Mimi………………………………………….. mzazi /milezi wa…………………………................... (mwanafunzi) nimeyasoma masharti yote yaliyomo katika fomu ya mwanangu kujiunga na shule ya sekondari Muungano Boys na ninakubali na kuahidi kwamba nitawajibika sawasawa kwa jambo lolote linalomhusu mwanagu. Aidha nitakuwa tayari kusimamia nidhamu ya mwanangu na kushirikiana na walimu kuhakikisha mwanangu anamaliza elimu ya kidato cha sita kwa mafanikio kwa kuwajibika kulipa michango ya shule pamoja na maelekezo megine yatakayokuwa yakitolewa na shule.

................................ .........................

Saini ya mzazi/Mlezi Tarehe

*Kiambatisho (e)*

**HALMASHAURI YA WILAYA YA CHATO**
**SHULE YA SEKONDARI MUUNGANO BOYS**
**MAELEZO BINAFSI YA MWANAFUNZI**

***FOMU HII IJAZWE NA MWANAFUNZI***

1. Jina kamili ……………………………………………………………………………………..........................

2. (a)Tarehe ya kuzaliwa………………………………………………………………………………........

(b)Mahali alipozaliwa…………………………………………………………………………………...

3.(a)Dini………………………………………………………………………………………………………...

(b)Dhehebu……………………………………………………………………………………………....

4. (a) Uraia……………………………………………………………………………………………...

(b) Kama siyo raia wa Tanzania taja uraia wako………………………………………………………

5. Shule ya sekondari uliyotoka………………………………………………………………………………

6. (a) Jina kamili la mzazi /mlezi………………………………………………………………………………

(b) Anwani ya mzazi/mlezi………………………………………………………………………………

(c) Kazi ya mzazi/mlezi…………………………………………………………………………………

(d) Kituo chake cha kazi……………………………………………………………………………...

(e) Namba ya simu………………………………………………………………………………………..

7. (a) Mahalia anapoishi………………………………………………………………………………

(b) Jina la mwenyekiti wa kitongoji/mtaa………………………………………………………………

8. (a) Je, unaishi na nani? Taja jina kamili …………………………………………………………....

(b) Je,una uhusihano gani na huyu uliyemtaja?..............................................................................

9.Ni yatima/si yatima……………………………………………………………………………......

10. Kama ni yatima mzazi yupi aliyefariki:mama/baba/wote………………………………………...

***Attachment (f)***

**CHATO DISTRICT COUNCIL**

MUUNGANO BOYS SECONDARY SCHOOL,
P.O.BOX 116,
CHATO.

Date.......................

**RE: REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION**

MEDICAL OFFICER IN CHARGE
............................................
.............................................

STUDENT NAME................................................................

Please examine the above named student as to his physical/mental fitness/unfitness for admission as fulltime student of Muungano Boys secondary school for academic year 2022/2023

The examination should include the following categories: Eye sight, Hearing, Epilepsy, Urine, Venerealdisease, Stool and any other body deformation

................
THE HEADMASTER

MKUU WA SHULE
MUUNGANO BOYS SEC. SCHOOL
S.L.P 6 CHATO

**RE: MEDICAL EXAMINATION RESULTS**

THE HEADMASTER,
MUUNGANO BOYS SECONDARY SCHOOL,
P.O.BOX116,
**CHATO.**

I have examined the above student and found him with the following disease/impairment/disabilities:
Eye sight.........................................................................................................
Urine examination...........................................................................................
Hearing............................................................................................................
Stool examination...........................................................................................
Speech ..........................................................................................................
Venereal diseases...........................................................................................
Limbs..............................................................................................................
Epilepsy..........................................................................................................
Additional information/other serious diseases...........................................................
..........................................................................................................................
Medical remarks..............................................................................................
..........................................................................................................................
Name and signature of attending
officer..............................Date.................................
Designation ..............................................Official stamp...............................................

**KIAMBATA CHA ZIADA**

**Ufafanuzi kwa mzazi kuhusu gharama za vifaa vinavyopatikana shuleni ni kama ifuatavyo:**

| Na | Kifaa | Gharama yake |
|---|---|---|
| 1 | SURUALI | @ 20,000 |
| 2. | T-SHIT (form six nzito yenye nembo ya moto) | 15,000 |
| 3. | SWETA yenye nembo | 12000 |
| 4. | TAI special ya kijani yenye mistari myeupe | 4000 |
| 5 | TRUCKSUIT | 18,000 |
| 6 | BUKTA NA TSHIRT YA MICHEZO | 10,000 |
| 9 | REAM PAPER A4 | 17,000 |
| 10 | EXAMINATION PAPER(ruled) | 13,000 |

**MUHIMU: Tutumie namba yako ya whatsapp INBOX kupitia nambari 0755375359 ili tukuunge kwenye group la wazazi wa watoto wa kidato cha V 2024.**